

Kupata chanjo ya COVID-19 katika kaunti ya King



Sasa tuna chanjo salama na Zenye ufanisi za kutukinga dhidi ya ugonjwa wa COVID-19.



Chanjo za COVID-19 zinapeanwa bure na zinapatikana bila kujali bima ya afya, uraia, au hali ya uhamiaji. Chanjo hii itasimamiwa/itagharamiwa na Medicare, Medicaid, kampuni za bima za kibinafsi. Na pia itagharamiwa kwa watu ambao hawana bima. Mhudumu wako wa afya hawezi kulipisha ikiwa utatembelea afisi yake kwa sababu ya kwenda kupata chanjo.



Uliza mhudumu wako wa afya utahitaji dozi ngapi, ili kuwa na ufanisi zaidi, chanjo ya Moderna na Pfizer zinahitaji dozi mbili, dozi hizo utapokea kati ya wiki tatu hadi nne zilizotengana, ilhali chanjo ya Johnson & Johnson inahitaji dozi moja tu.



Chanjo za COVID-19 ni salama na zenye ufanisi mkubwa. CHANJO ZOTE ZA COVID-19 ni lazima zipitie hatua kali za majaribio na tathmini kabla zikubalike kutumika. Shirika la Marekani linalohusika na usimamizi wa chakula na dawa (FDA) iliidhinisha matumizi ya chanjo kwa matumizi ya dharura na hawakupata matatizo yoyote ya kiusalama. Wataalamu wa kujitegemea walidhibitisha kwamba chanjo zinafikia viwango vya juu vya kiusalama na ufanisi.



Unaweza hisi/kupata athari baada ya chanjo. kama chanjo zingine za kawaida, unaweza kuvimba mkono, kupata homa, maumivu ya kichwa, au uchovu baada ya kupata chanjo. Hizi ni ishara kwamba kinga ya mwili wako inajenga ulinzi.



Weka kila mmoja salama baada ya kupata chanjo. Wakati chanjo itazuia watu wengi kuwa wagonjwa, tungali tunajifunza ni namna gani mwafaka chanjo inazuia maambukizi ya COVID-19. Endelea kuvaa maski/barakoa, kaa umbali wa futi sita (mita mbili), na uangalie mwongozo wa Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia magonjwa (CDC) kuhusu watu ambao wamepokea chanjo yote: bit.ly/fully-vaccinated

JINSI YA KUPATA CHANJO

Kwa mara ya kwanza, vifaa vya chanjo ya COVID-19 vitakuwa chache katika jimbo na nchi nzima. Chanjo itatolewa kwanza kwa vikundi maalumu vilivyo katika hatari kubwa, kama wafanyakazi wa huduma ya afya, wazee, na watu ambao wamo katika mazingira ambayo yana watu wengi/mikusanyiko.

Kuanzia Aprili tarehe kumi na tano mwaka wa 2021, mtu yeyote mwenye umri wa miaka kumi na sita na zaidi atastahiki kupata chanjo.

Kwa sasa vifaa vya Chanjo na kujiandikisha/kujisajili kunapatikana kwa uchache mno. Chanjo itapatikana kwa watu wengi kadri ugavi unavyoongezeka. Hatimaye, kila mtu ambaye anataka chanjo ataweza kupata chanjo hiyo.

Jinsi ya kupanga kujisajili/kujiandikisha

Njia za kujisajili ikiwa unastahiki kupata chanjo:

- 1) **Pigia simu ofisi ya daktari wako au mhadumu wako wa afya** ili ujue ikiwa wanaandikisha/kusajili watu ili wapokee chanjo.
- 2) Tumia kifaa cha kutafutia chanjo cha jimbo la Washington (chagua lugha katika menyu kunjuzi ya kona ya juu kulia): [VaccineLocator.doh.wa.gov](https://vaccineLocator.doh.wa.gov)
- 3) **Unahitaji usaidizi ili kujiandikisha/kujisajili kupata chanjo kupitia kwa simu?** Piga simu kwa kituo cha simu cha COVID-19 cha kaunti ya King siku yoyote kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa moja usiku kwa nambari 206-477-3977. Wakalimani wanapatikana – sema lugha unayohitaji wakati wa mawasiliano.

Kwa maelezo zaidi kuhusu ni nani anaweza kupata chanjo sasa na namna ya kupata chanjo: tembelea tovuti ya [Kingcounty.gov/vaccine](https://kingcounty.gov/vaccine)

USAFIRI HADI MAHALI ULIPOJIANDIKISHA KUPATA CHANJO

- Kwa usaidizi kupitia kwa simu, piga simu kwa nambari ya simu ya usaidizi inayoratibu usafirishaji wa chanjo kwa nambari **425-943-6706 Jumatatu-Ijumaa kati ya saa mbili u nusu asubuhi hadi saa kumi jioni. Bonyeza nambari tano ili kupata wakalimani.** Unaweza kuwacha ujumbe wa sauti na utapigiwa simu.
- Ili kuomba usafirishaji wa watu wengi, tafadhali tembelea tovuti ifuatayo (inapatikana kwa kiingereza tu): bit.ly/vaxride
- Ili kujiifunza kuhusu chaguzi za usafirishaji, pamoja na usafirishaji wa wazee, walemavu, wanaopokea huduma za Medicaid, na wakongwe tembelea tovuti ya: FindARide.org/COVID